

**OFISI YA RAIS TAWALA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA BUSOKELO**



**SHULE YA SEKONDARI YA  
WASICHANA BUSOKELO,  
S. L. P. 506,  
TUKUYU,**

Email: [bgsskandete@gmail.com](mailto:bgsskandete@gmail.com)  
Simu: 0764818574/0757021255

KUMB Na. BGSS/S. 5087/J.O/20.

12.12.2020

**JINA LA MWANAFUNZI .....**  
**S.L.P .....**

.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA  
BUSOKELO ILIYOPO WILAYA YA RUNGWE MKOANI MBEYA KWA MWAKA  
2021.**

**1.0 UTANGULIZI:**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari YA WASICHANA PEKEE BUSOKELO Mwaka **2021**. Shule hii ni ya hostel (Daharia) na ipo Nyanda za juu kusini mwa Tanzania mkoa wa mbeya wilaya ya RUNGWE-BUSOKELO

Shule hii ipo katika mji mdogo uitwao Kandete umbali wa km 25 kutoka makao makuu ya Halmshauri ya Wilaya Busokelo. Aidha, kwa kupitia Katumba shule ipo umbali wa km 31 kutoka Tukuyu Mjini.

Huduma zinazopatikana shuleni ni pamoja na maji, simu, umeme na afya ambapo Kituo cha afya kipo km 1. toka shuleni.

Masomo ya taanza rasmi tarehe **11/01/2021** kwa Kidato cha Kwanza unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **04/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **11/01/2021**.

**KAULI MBIU YA SHULE HII: "ZEAL AND CONSTANCY EDUCATION"**

**2.0 Mambo muhimu ya kunzingatia**

**2.1 SARE ZA SHULE.**

**2.1.1 MAVAZI YA DARASANI.**

- Gauni mbili **(2)** aina ya solo fupi rangi nyeupe zifike juu ya magoti zenye marinda chini na shingo ya duara, zote mbili zitashonwa shuleni kwa jumla ya Tsh **32,000/=**.
- Suruali mbili **(2)** rangi ya ugoro zitashonwa shuleni Kwa Tsh **41,000/=**( Gharama ya kitambaa na kushona)

- Hijab nyeupe kwa wanafunzi wakiislam zisizokuwa na urembo.
- Sweta moja rangi ya ugoro litakalopatikana shuleni kwa shs. **10,000/=**
- Viatu vyeusi vya kamba jozi mbili **(02)** visivyo na visigino virefu aje navyo mwanafunzi.
- Soksi nyeupe jozi nne **(4)** au zaidi aje nazo mwafunzi

### **2.1.2 MAVAZI NJE YA DARASA**

- Gauni mbili (2) (shamba dress) rangi ya *dark blue* zitakazopatikana shuleni kwa jumla ya Tsh. 59,000/=.
- Sweta la *dark blue* (litapatikana shuleni ) yote Tsh **20,000/=**
- T-shirt ya dark blue yenye nembo ya shule itapatikana shuleni kwa Tsh **13,500/=**
- “Track suit” jozi mbili (2) moja rangi ya **dark blue** na nyingine rangi ya **kijivu** zote zitapatikana shuleni kwa Tsh **36,000/=**
- Aje na Raba nyeupe za michezo
- Aje na Soksi nyeusi jozi **2** za michezo
- Aje na nguo za michezo rangi ya bluu (*Tshirt na Bukta*) zinazomtosha vizuri bila kubana na zisizo na maandishi mengi.
- Hijabu ya *dark blue* kwa waislam isiyokuwa na urembo
- Koti moja jeusi lisilo na maandishi kwa ajili ya kujistili na baridi aje nalo mwanafunzi.
- Aje na Viatu vya wazi (sandals au kandambili ) kwa ajili ya kuogea/ kuvaa wakati wa shughuli za nje.

**KUMBUKA: Ili kuleta mfanano na kulinda maadili unaagizwa kuzingatia kuwa mavazi yote yaliyoainishwa kupatikana shuleni yakitolewa kwa gharama zilizoainishwa na shule na si vinginevyo.**

### **2.2 Vifaa vya darasani:**

- a) Madaftari makubwa kumi **(10)** – (Counter books quire **3**).
- b) Kalamu za wino na Risasi za kutosha, mifuto, kichongeo na rula
- c) Mkebe (Mathematical set) na Kikokotoo (Calculator) ya kawaida
- d) Graph pad moja.
- e) Daftari ndogo kumi na mbili **(12)** kwa ajili ya mazoezi.
- f) Rimu A4 mbili **(2)** moja iletwe muhula wa I na nyingine muhula wa II kwa ajili ya mitihani na majaribio mbalimbali.
- g) Picha (*passport size*) nne (4) za rangi (Kwa kutumia kitambaa cha bluu bahari nyuma).
- h) Saa ya mkononi moja (1)
- i) Aje na Dictionary English-English (Kamusi ya kiingereza) 1 kwa matumizi yake.

### **2.3 Mahitaji binafsi ya bwenini:**

- a) Blanketi moja (1) mashuka manne **(4)** mawili pinki na mawili (2) light blue
- b) Mto mmoja na foronya mbili za pink na light blue.
- c) Ndoo 2 kwa ajili ya kuogea na kufulia ( na kigaloni /kidumu cha lita 5)

- d) Sanduku la chuma (Tranker).
- e) Kanga mbili(2) au vitenge 2
- f) Pedi za kutosha
- g) Godoro moja futi 2.5 x 6
- h) Mwavuli mmoja, bakuli, kijiko na kikombe cha uji.
- i) Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa au uthibitisho wowote wa uraia.
- j) Chandarua kwa ajili ya kujikinga na mbu.

**MUHIMU: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo nyingine za aina yoyote ambazo haikuagizwa katika fomu hii.**

**2.4 Vifaa vya kazi na usafi**

- a) Ufagio mgumu (*hard bloom*) mmoja 1
- b) Ufagio laini (*Soft bloom*) mmoja 1
- c) Kwanja 1 lililonolewa vizuri.
- d) Jembe moja lenye mpini
- e) Ufagio wa chelewa 1

**NB: Vifaa vyote vitakaguliwa kabla hujaingia bwenini/hosteli.**

**2.5 MAJUKUMU YA MZAZI/MLEZI**

**KWA KUZINGATIA WARAKA WA ELIMU NAMBA 6 WA MWAKA 2015 KUHUSU UTEKELEZAJI WA ELIMU MSINGI BILA MALIPO, MZAZI/MLEZI ATAKUWA NA MAJUKUMU YAFUATAYO.**

- (i) Kununua sare za shule na michezo, vifaa vya kujifunzia vikiwemo madaftari na kalamu, na chakula kwa wanafunzi wa kutwa.
- (ii) Kugharamia matibabu kwa watoto wao.
- (iii) Kulipia nauli ya kwenda Shule na kurudi kwa wanafunzi wa kutwa na wanafunzi wa bweni wakati wa likizo.
- (iv) Kununua magodoro, shuka vifaa vya usafi binafsi kwa wanafunzi wanaosoma Shule za bweni na wanaoishi katika Hosteli zinazotumiwa na serikali, na
- (v) Kukemea na kutoa taarifa kuhusu mienendo inayokwenda kinyume na elimumsingi bila malipo.

Kwa kuwa shule ya Sekondari WASICHANA BUSOKELO ni shule ya hostel gharama za chakula na hostel zimeambatanishwa.

**3.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

Mzazi au Mlezi ahakikishe amesoma kikamilifu sharia za shule na mchanganuo wa gharama za chakula. Aidha, ahakikishe amejaza kikamilifu hati ya mzazi ya kukubali masharti ya shule, fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) na taarifa binafsi ya mwanafunzi.

**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. **25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. **10** ya mwaka 1995 Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais -TAMISEMI YENYE JUKUMU LA Usimamizi na Uendeshaji Elimu Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

- a) Heshima kwa viongozi Wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima:
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima:
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation),
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa,
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii,
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule,
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa,
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na
- i) Kutunza mali za umma.
- j) Hurusiwi kuwa na **simu** wala kamera.

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE:**

- a) Wizi.
- b) Uasherati na Ushoga.
- c) Ubakaji.
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevywa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi,kubeli na kadhalika.
- e) Kupigana au Kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kudharau Bendera ya Taifa.

- h) Kuwa mjamzito/Kupata mimba.
- i) Kuoa au Kuolewa.
- j) Kutoa mimba.
- k) Kugoma kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na Usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- m) Kutoroka Shule au kulala nje ya Shule bila ruhusa.
- n) Kutokuwepo shuleni bila ruhusa kwa muda wa siku **30** mfululizo.
- o) Kumiliki simu ya mkononi

#### 4.0 **AFYA YA MWANAFUNZI.**

- 4.1 Huduma ya kwanza hutolewa shuleni kabla ya mgonjwa kupelekwa hospitali kwa matibabu zaidi.
- 4.2 Tunaomba Mzazi/Mlezi uwe muwazi katika kutoa taarifa za mtoto wako kuhusu hali halisi ya afya yake. Ikiwezekana vyeti vya matatizo ya kiafya kutoka kwa daktari vikabidhiwe kwa Mkuu wa Shule kwaajili ya uthibitisho.
- 4.3 Ni LAZIMA mwanafunzi awe na kadi ya **bima ya afya pamoja** pesa kiasi cha shilingi **20,000/= (Elfu ishirini tu) itakayobidhiwa shuleni moja kwa moja kwaajili ya gharama za usafiri wa dharura.**
- 4.4 Mwanafunzi haruhusiwi kutunza dawa Bwenini **bila idhini.**
- 4.5 Mwanafunzi haruhusiwi kuja na dawa ya miti shamba shuleni.

**Kiambata Na. 2**

<b>7.0 MCHANGANUO WA GHARAMA ZA CHAKULA KWA KILA MWANAFUNZI</b>							
S/N	AINA YA CHAKULA	KIASI KWA MWANAFUNZI 1 KWA MLO (KG/LITA/FUNGU)	IDADI YA MILO KWA WIKI	JUMLA KWA WIKI 1 (KG/LITA/FUNGU)	JUMLA KWA WIKI 40 (MWAKA)	BEI KWA(TSH)	GHARAMA (TSH)
1	MICHELE	0.25	2	0.5	20	2000	40,000
2	MAKANDE	0.25	3	0.75	30	1,000	30,000
3	MAHARAGE	0.125	14	1.75	70	2000	140,000
4	UNGA (Ugali +Uji)	0.276	9	2.484	99.36	1,500	149,040
5	NYAMA	0.125	1	0.125	5	5,000	25,000
6	MAFUTA	0.0068	14	0.0952	3.808	4000	15,232
7	CHUMVI	0.0051	14	0.0714	2.856	1,000	2,856
8	SUKARI	0.025	7	0.175	7	2,800	19,600
9	MBOGA ZA (MAJANI)	0.25	2	0.5	20	400	8,000
10	MATUNDA	pc			1		4,000
11	VITUNGUU	kg			1	3000	1,700
12	NYANYA				1	6000	3,400
13	KUNI				1	100,000	100,000
	JUMLA						<b>542,728/=</b>

**ZINGATIA**

4.6 Mwanafunzi anatakiwa kula chakula kinachotolewa na shule. Shule haitoi chakula **maalumu** ( special diet ) na mwanafunzi haruhusiwi **kujipikia**

4.7 Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vyakula shuleni au kuletewa kutoka nje ya shule .

**5.0 MCHANGANUO WA GHARAMA ZA HOSTEL KWA KILA MWANAFUNZI**

- Malipo ya watumishi ( Mpishi, Mlinzi, Matron na Katibu muhtasi) .....39,300/=
  - Umeme .....2,000/=
  - Matibabu .....15,000/=
  - Tahadhari.....10,000/=
  - Kuhifadhi taka .....4,250/=
  - Vifaa vya jikoni ..... 5,000/=
  - Ukarabati .....6,000/=
  - Mawasiliano .....2,500/=
  - Kitambulisho .....5,000/=
  - Ushindani kitaaluma .....10,000/=
- JUMLA KUU TSH                    99,050/=**

<b>CHAKULA</b>	<b>542,728/=</b>
<b>HOSTELI</b>	<b>99,050/=</b>
<b>JUMLA</b>	<b>641,778/=</b>

## 6.0 NAMNA YA ULIPAJI

- Fedha itakayolipwa kwenye Akaunti ya Benki kwa awamu nne kwa mwaka mzima ni kwa ajili ya Chakula na Hosteli kama ifuatavyo:

Awamu I JANUARI	200,000	<b>ILIPWE KWENYE AKAUNTI BENKI NMB</b> NAMBA YA AKAUNTI: <b>63710000367</b> JINA AKAUNTI: <b>SEKONDARI YA</b> <b>WASICHANA BUSOKELO</b>
Awamu II MACHI	100,000	
Awamu III JULAI	200,000	
Awamu IV SEPTEMBER	141,778	
<b>JUMLA</b>	<b>641,778</b>	

- Fedha/ michango mingine itakayolipwa moja kwa moja shuleni ni kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:

1. Kwa ajili ya usafiri wa dharula	20,000	} ILIPWE MOJA KWA MOJA SHULENI
2. Walimu wa muda Tsh	28,000/=	
3. Mavazi ya Mwanafunzi Tsh	201,500/=	
<b>JUMLA</b>	<b>249,500/=</b>	

***N.B. MWANAFUNZI HATAPOKELEWA BILA HATI YA MALIPO YA BENKI  
(BANK PAY IN SLIP)***

***UNAPORIPOTI NJOO NA FOMU HII  
NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA KARIBU SANA SHULE YA  
SEKONDARI YA WASICHANA BUSOKELO.***

IMEANDALIWA NA:

TUMTUKUZE ELIA MPINDO  
**MKUU WA SHULE**  
**0764818574**

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO**

**SIMU Na. 0764818574.**  
EMAIL: [bgsskandete@gmail.com](mailto:bgsskandete@gmail.com)



ANUANI YA MZAZI  
.....  
.....  
.....  
.....

Kumb. Na. BGSS/FS/554/VOL3

Tarehe.....

SHULE YA SEKONDARI YA  
WASICHANA BUSOKELO,  
S. L. P. 506,  
**TUKUYU.**

K.K. MKUU WA SHULE,  
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BUSOKELO,  
S.L.P 506,  
**TUKUYU.**

**YAH: HATI YA KUKUBALI MASHARTI KUHUSU MTOTO WANGU KUSOMA  
SEKONDARI YA WASICHANA BUSOKELO**

Mimi.....  
..... Mzazi/mlezi wa mwanafunzi .....  
aliyekuwa akisoma shule ya msingi..... katika  
Wilaya ya .....

Ninakubali mtoto wangu asome shule ya sekondari YA WASICHANA  
BUSOKELO ilioko Wilaya ya Rungwe kwa kufuata masharti yafuatayo,

1. Kwamba mtoto wangu atahudhuria masomo kama kawaida kufanya shughuli nyingine zote za shule tangu kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne, na atazingatia sheria na taratibu zote za shule.
2. Nakubali masharti na gharama zilizotolewa katika barua ya kuitwa kwa mwanafunzi (Joining instructions) na nitayatimiza kwa wakati unaotakiwa.
3. Nitahakikisha atafika shuleni kwa kufuata tarehe zilizopangwa kwa kipindi chote cha miaka minne.

**SAINI YA MZAZI/MLEZI..... TAREHE .....**



**TAARIFA BINAFSI**

1. Jina kamili la mwanafunzi .....

2. Jina kamili la mzazi .....

Anuani kamili .....

Namba ya simu .....

Mkoa .....

3. Majina ya watu watatu ambao mawasiliano ya kiofisi kuhusu mwanafunzi husika yatafanyika.

<b>JINA</b>	<b>UHUSIANO</b>	<b>NAMBA YA SIMU</b>
-------------	-----------------	----------------------

1. ....	.....	.....
---------	-------	-------

2. ....	.....	.....
---------	-------	-------

3. ....	.....	.....
---------	-------	-------

4. Jina sahihi la mzazi/mlezi

Jina.....	Sahihi .....
-----------	--------------

5. Jina kamili la afisa mtendaji

Jina .....	Sahihi .....
------------	--------------

6. Taarifa hii irudishwe kwa mkuu wa shule ya Sekondari YA WASICHANA BUSOKELO.

**TUMTUKUZE ELIA MPINDO  
MKUU WA SHULE  
0764818574**

**MEDICAL CERTIFICATE FORM**

STUDENT NAME.....

To be completed by a Government Medical Officer or a doctor from a recognized health institution in respect of form one entrant. Please examine the above as to her/his physical and mental fitness as a student at this school.

The examination should have to involve the following categories

1. Vision with glasses right ..... left.....
2. Blood pressure .....
3. Hemoglobin .....
4. F. V. Bleeding .....
5. Urine for sugar. ....
6. Stool for routine examination .....
7. Venereal diseases .....
8. Neurosis .....
9. T. B. Test .....
10. Any abnormality
  - a) Heart .....
  - b) Lung .....
  - c) Spleen .....
  - d) Chest .....
11. Is there any serious disease e.g. Leprosy, Epilepsy, Asthma, Diabetes .....

Doctor's name.....

Signature and official stamp

.....

Date .....